KISWAHILI
Karatasi 3
Fasihi
Julai/Agosti 2014
**Muda: Saa 2½**

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA WESTLANDS

**KISWAHILI**
Karatasi 3
Julai/Agosti 2014
**Muda: Saa 2½**

**MAAGIZO**

* Jibu maswali **manne** pekee.
* Swali la kwanza ni la **lazima**.
* Chagua maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizobaki, yaani Hadithi fupi, Fasihi Simulizi na Ushairi
* Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.
* Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. “Watu wenye matumbo yasiyotulia huwa akili zao nazo hazitulii ..... jambo hili ni hatari kwa kiongozi yeyote ...”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza chanzo cha hatari inayozungumziwa. (alama 6)

c) Msemaji anatoa tahadhari kwa msemewa. Ifafanue. (alama 4)

d) Msemewa anachukua hatua ipi kukabiliana na ujumbe huu. (alama 4)

e) Eleza mbinu inayojitokeza katika usemi huu. (alama 2)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B : RIWAYA**
**Said A. Mohamed : Kidagaa Kimemwozea**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. Jumuiya ya Tomoko ni kioo halisi cha matatizo yanayokumba mataifa yanayoendelea. Thibitisha. (alama 20)

3. Lo! Kumbe sumaku ya kaburi yaniotea ili kuanza kunivuta vuu kama kijembe!

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Taja mbinu **tatu** za lugha kwenye dondoo na utoe mifano. (alama 6)

c) Eleza maudhui yoyote **matatu** yanayoashiriwa na dondoo hili. (alama 6)

d) Eleza mifano ya wahusika wengine **wawili** waliovutwa na sumaku ya kaburi. (alama 4)

**SEHEMU C : HADITHI FUPI**
**K. Walibora na S.A Mohamed : Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. “Shangazi wakumbuke watoto. Waonee huruma!”

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b) Fafanua mbinu ya kisanaa inayodekezwa katika nukuu hii. (alama 2)

c) Jadili jinsi aina ya uovu unaodokezwa katika dondoo hili ulivyoendelezwa na wahusika wengine katika hadithi husika. (alama 6)

5. Jadili ufaafu wa anwani ya “Mizizi na Matawi” na uitolee mifano mwafaka kutoka kwa hadithi yenyewe.

ii) Taja na ufafanue dhima zozote **nne** za vichekesho katika jamii. (alama 8)

**b)** i) Maapizo ni nini ? (alama 2)

ii) Jadili sifa zozote **nne** za maapizo. (alama 8)

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU YA E : USHAIRI

**7. Soma shairi ulilopewa kisha ujibu maswali yanayofuata.**

1. Nisukume kiberenge kikwee mlima
Mkoi wangu kaa kitako usikilize
Ninakuhamu wewe na Kyumbo wa mama (jamaa yangu)
Simu hiyo ilipigwa alfajiri
Ikaingia kituoni haraka
Gari moshi ya Nyeri tuisubiri

2. Niundiwe uta na kudai kipande
Pindi ujapo nataka uende haraka
Mpaka alipo Mbenya, ashindapo umwone
Umweleze kwamba natamani aniletee salamu

3. Wazungu ni katili huwafunga watu
Kwa pingu nyeusi kama kaniki
Na uthubutupo kuzionyesha utundu,
Utatambua kuwa zimekupiku
Zimeundwa zitoshee maungo
Nauliza je, ni mkono wa mtu uliufungwa hivi ?
Ama ni utundu wa wazungu waliojaribu hivi ?

4. Nilifungwa pamoja na Kivandi
Na wale wazungu wa Machakos wenye nishani
Wadhanio kuwa Nairobi ndipo penye suluu ya
Wafungwa

5. Tulalapo tulitetemeka,
Kutokana na baridi ya mzizimo ya Machakos
Niliona wazee wa umri wa babangu wakiteseka
Wakiteseka mpaka nikajiwa na machozi
Nikimwuliza Ndetei, disii kuwanyima watu mlo
Nikamwambia gusa hapa, uone ulipo ujanja
Siku hiyo nilijua dhiki ya kuwa kifungoni

6. Ngelema na Kalanzo
Nimesikia siku hizi unashinda na tasa
Ninadadisi na kujuzwa kuwa umeolewa

7. Siku nitakapotokeza tena huko nyumbani
Nilimwonapo Mbenya nitaangua cheko aaa!
Kisha nimweleze vuta ugoro kwanza, tusalimiane

**Maswali**

a) Eleza utungo huu ni wa aina gani kwa kutoa ushahidi ? (alama 5)

b) Fafanua dhamira **tano** za mshairi ambazo ameibua kwenye shairi. (alama 5)

c) Andika ubeti wa **nne** kwa lugha tutumbi. (alama 4)

d) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 4)

e) Taja na ueleze mbinu mbili za uandishi ambazo zimejitokeza katika shairi hili. (alama 2)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com